# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI**
**JULAI/AGOSTI 2025**
**KARATASI YA 3**
**FASIHI**
**KIDATO CHA TATU**

**Swali la Kwanza**

**USHAIRI:**
**Soma shairi kisha ujibu maswali.**

1. Tunda la elimu zote, wanasema wanazuoni
   Ni kwamba mtu apate, kumtambua manani
   Ndipo hadhi apate, akumbukwe duniani.

2. Elimu bila zote, haizidi asilani
   Giza na nuru nuhali, kitu havitangamani
   Uwongo ufe kweli, itue nuru moyoni.

3. Elimu ni kama mali, haichoshi kutamani
   Ni bora yashinda mali, taji la wanazuoni
   Elimu njoma miali, langazayo gizani.

4. Mtu hachomwi na mwiba, na viatu miguuni
   Ulimwenguni una miiba, tele majiani
   Elimu ukiishiba, u salama duniani.

5. Wafu ni wasiosoma, watazikwa ardhini
   Hai ndio maulana, wapaao maangani
   Elimu jambo adhima, aso nayo maskini.

6. Toa wakfu ujana, elimu ukutamani
   Na uwe mzee sana, kujua usijihini
   Elimu ni jambo adhima, aso nayo maskini.

7. Elimu ina malipo, utayalipwa mwishoni
   Pale uitafutapo, utayalipwa mwoshini
   Mwanachuoni afapo, mbingu huwa na huzuni.

8. Haki ya kuheshimiwa, ni yao wanachuoni
   Wao wameongolewa, na ni taa duniani
   Kweli wanapoijua, watoe bila kuhuni.

9. Elimu bila amali, mti usio majani
   Haumtii kivuli, aukaliaye chini
   Inakuwa mashkeli, wa kughuri insani.


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**Maswali**

a) Toa kichwa mwafaka kwa shairi hili. (al 2)
**Elimu**

b) Taja na ueleze aina bahari za shairi. (al 3)
- **Aina – tathlitha – mishororo mitatu**
- **Bahari - i) ukara – Vina vya mwisho vinatiririka na vya kati vinabadilika kila ubeti. Mathnawi – vipande viwili.**

c) Eleza umbo/ muundo wa shairi. (al 4)
- **Shairi lina beti tisa (9)**
- **kila ubeti una mishororo mitatu**
- **vina vya mwisho vinakaririwa (ni) na vya kati vinabadilika kila ubeti.**
- **Mizani ni kumi na sita 16(-8-8) kila mshororo**
- **Shairi halina kibwagizo**
- **Shairi lina vipande viwili**

d) Fafanua maudhui katika ubeti wa tatu na wa saba. (al 6)

**<u>Ubeti wa tatu (3)</u>**
- **Elimu ni kitu cha umuhimu sawa na mali ambayo hutamani.**
- **Elimu inashinda mali na hata ni bora kushinda shahada ya chuoni.**
- **Elimu hutoa mwangaza katika giza.** **(3x1 = 3)**

**<u>Ubeti wa saba (7)</u>**
- **Elimu inakulipa baada ya kuipata.**
- **Wakati unasoma/unatafuta elimu usitarajie mambo yawe mepesi.**
- **Mwanafunzi akifa, watu huhuzunika.**

e) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha ya nathari. (ala 3)
- **Mwandishi anasema elimu ambayo haina matokeo/ faida ni sawa na mti ambao hauna matawi.**
- **Itakuwa haimsitiri mtu aliyeketi chini yake kutoka kwa jua/ haimpi kivuli kumzuia iyeketi keti chini yake kuchomwa na jua.**
- **Elimu isiyosaidia/ bila faida inakuwa na kasoro kwa kumwendeleza binadamu.**

f) Tambua mbinu yoyote ya lugha inayojitokeza katika shairi.
- **Takriri – neno elimu limerudiwa.**

**SWALI LA PILI**

**<u>Fasihi simulizi</u>**

a) Fafanua aina zifuatazo za nyimbo. (ala 6)

i) Nyiso
**Nyimbo za tohara huimbwa wakati wa tohara au katika shughuli za jando.**

ii) Nyimbo za siasa
**Nyimbo zinaimbwa wakati wa siasa/ katika shughuli za siasa.**

iii) Bembelezi
**Nyimbo zinazoimbiwa watoto na mlezi ili kuwabembeleza wanyama au kuwaon'oa walale.**

b) Fafanua umuhimu wa nyimbo. (alama 10)
- **Hutumiwa kuburudisha jamii na waimbaji**
- **Huwasilisha ujumbe maalum**
- **Huhifadhi na kuendeleza utamaduni na historia ya jamii**


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

- **Hufunza maadili/ adabu katika jamii**
- **Hurekebisha tabia katika jamii**
- **Huhamisha watu katika jamii kuhusu ukweli, haki uwajibikaji nk.**
- **Hukuza au kuendeleza lugha**
- **Hutumiwa kuonya na kutahadharisha**
- **Ni kutega uchumi/ ajira – watu wengine hupata riziki kutokana na uimbaji.**
- **Hukuza umoja/ ushirikiano katika jamii**
- **Huliwaza na kufariji hasa wakati wa majonzi**
- **Huzindua jamii kuhusi mambo Fulani**
- **Huhimiza jamii kufanya mambo Fulani (kazi)**

**(10 x 1 = 10)**

c) Fafanua umuhimu wa nyimbo katika utambaji wa hadidhi. (al 4)
- **Huondoa uchovu/ ukinaifu**
- **Hushirikisha hadhira**
- **Kutanganisha matukio**
- **Kurefusha hadidhi**
- **Kusisitiza ujumbe katika hadidhi kuburudisha hadhira** **(4x1=4)**

**SWALI LA TATU**

**<u>Tamthilia ya bembea ya maisha</u>**

"Eti alama! My foot! Eti ameshika nafasi darasani lakini akapandisha alama…………"

a) i) Nani alisema maneno haya? (alama 1)

**Banju**

ii) Nani alikuwa akiambiwa maneno haya? (alama 1)

**Neema**

iii) Walikuwa wapi? (alama 1)

**Nymbani kwao**

iv) Kwa maneno haya yakasemwa? (alama

**Banju aliona kuwa lemi alifanya vibaya masomoni ilhali Neema aliona alifanya vizuri.**

b) Jadili sifa za mnenaji. (alama 10)
- **Msiri – ana madeni mengi lakini hamwambii hata mkewe, Neema**
- **Mchapa kazi/ mwenye bidii – anaenda kazini hata Jumamosi.**
- **Mwepesi wa hasira – anakasirika anapoambiwa kuwa Lemi alifanya vizuri.**
- **Mwenye hisani – anasaidia Neema kupata matibabu hata kama hakumjua.**
- **Mtamaduni – anaamini kuwa si sawa Sara hakulala kwake.**
- **Mwajibikaji – analipia mahitaji yote yak wake.**
- **Mwenye kutamauka – amepoteza matumaini na Lemi.** **zozote(5x2=10)**

c) Ni nini umuhimu wa anayeambiwa maneno haya? (alama 6)
- **Anawakilisha wanawake ambao ni wasomi katika jamii inayotawaliwa na wanaume.**
- **Ni kielelezo cha watoto wanaowajibika kwa kuwasaidia wazazi wake.**
- **Anasimamia wanawake wambao wametekwa na usasa kwani anakumbatia mambo mengi ya kisasa.**
- **Anawakilisha wanawake wenye bidii – anaamka mapema kwenda kazini na kurudi akiwa amechelewa.**



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

- **Ni kielelezo cha watu wenye mapenzi ya dhati – anampenda mama yake Sara anafanya kila kitu kuokoa maisha yake anapougua.** **Zozote (2x3=6)**

**SWALI LA NNE**

**Tamthilia ya Bembea ya Maisha**

Bembea ya Maisha ni tamthilia inayohimiza mshikamano wa kijamii. Toa hoja zinazounga mkono kauli hii. (alama 20)

- **Beni ya Yona wanakuja kuwa Luka kula na kunywa pamoja.**
- **Dina anakuja kwa Sara ili kusaidia kupika**
- **Luka anamaliza mzozano baina ya Yona na Beni kuhusu taaluma ya mwanawe Beni.**
- **Banju anagharamia masomo ya salome**
- **Banju anamhifadhi Salome akiwa anasoma**
- **Banju anamnunulia Neema gari**
- **Banju anapiga jeki matibabu ya Sara**
- **Banju anashirikiana na Neema kujengea wazazi wa Neema nyumba**
- **Banju anampeleka Neema hospitalini na kugharamia matibabu yake**
- **Banju anamsaidia Neema kulea Lemi na kufanya kazi za nyumbani**
- **Neema anawanunulia wazazi wake jik la gesi**
- **Neema anabeba Sara kwa gari lake hadi hospitalini na kurudisha nyumbani**
- **Asna anamhifadhi Sara kwake na kumpika**
- **Yona anashirikiana na Sara kulea mabinti zao**
- **Yona anatambua mchango wa Neema kusimamia mji wake na kumshukuru.**
- **Yona huhudhuria mikutano ya vyama**
- **Yona anaandaa kiamshakinywa na kumgoja Sara wafungue pamoja**
- **Neema anatumia babake Yona pesa za dawa za kustarehe na wazee wengine.**

**Zozote (2x10=20)**



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes